



KILIMO THABITI

KILIMO KINACHOHIMILI MABADILIKO YA TABIA NCHI



Kuhusu Mradi wa Kilimo Thabiti

Taasisi ya utafiti wa kilimo Tanzania (TARI), shirika la Tanzania Youth Espouse for Gender and Development (TYEGD), kampuni ya Esoko Tanzania, na kampuni ya Weather Impact, kwa pamoja, wanatekeleza mradi wa Kilimo Thabiti, wenye lengo la kuwawezesha wakulima 2,400 wa mahindi na Muhogo, kupata taarifa zinazolenga kanuni bora za kilimo na ushauri wa hali ya hewa, katika wilaya za Bunda na Butiama, Mkoa wa Mara

Katika utekelezaji wa Mradi wa Kilimo Thabiti, tumetoa mafunzo kwa wakulima 500 kuhusu mbinu bora za kilimo na matumizi ya taarifa za hali ya hewa, kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na uwakilishi wa vijana. Tunaboresha huduma zetu na kupima athari kupitia mfumo imara wa kukusanya taarifa



Ubunifu Wetu

Ushauri wetu wa hali ya hewa wa kilimo ni mfumo wa kipekee unaotuma ujumbe mara mbili kwa wiki katika muundo wa SMS ambao umeundwa mahsusi kwa ajili ya mahindi na/au zao la muhogo kwa kila mkulima aliyesajiliwa. Usajili wa wakulima ni bure

Taarifa ya hali ya hewa na Mazingira

- Taarifa ya utabiri wa hali ya hewa
- Taarifa ya hali ya hewa kuanza kupanda
- Vipimo vya unyevu na mvua

Taarifa za Kilimo

- Mbinu bora za kilimo zinazopendekezwa
- Taarifa za aina ya mazao na vigezo vingine

Taarifa mahususi za mkulima

- Mazao yaliyolimwa na tarehe za kupanda
- Eneo halisi la mashamba
- Mkakati wa mbolea
- Lugha

Oct03, Upandaji Msimu wa kilimo unakaribia. Eneo lako linatarajiwa kupata mvuanyingi kufikia Alhamisi ijayo. Unashauriwa kupanda MAHINDI/MUHOGO: [-]

Apr19, Hadji Jpili: mkubwa uwezekano kidogo (16mm ndani ya siku3). Baada ya Jpili: kuna uwezekano mkubwa (76% wa mvua kidogo (24mm ndani ya siku4)

Mei15, Mahindi yanaweza kuwa yamekaribia kukomaa. Unaweza kuvuna wakati wa kiangazi ikiwa majani yanageuka kuwa ya njano na kukauka. Utabiri wa hali ya hewa kuanzia Ijumaa, ndani ya siku 9 zijazo

Vidokezo

Mfumo wa kukusanyia Taarifa

Mfumo wa mAgric Colekt uliotengenezwa na kampuni ya Esoko unaruhusu ukusanyaji wa taarifa kidijitali katika lugha mbalimbali:

- Tafiti za msingi za mwanzo na mwisho
- ukuaji na ufuatiliaji wa afya ya mmea
- vipimo vya eneo husika kwa wakulima

Dashibodi ya Ufuatiliaji

Taarifa inaonyeshwa katika muda halisi kwenye dashibodi ya Kilimo Thabiti



Wakulima Wanasayansi

Kundi la wakulima wanasayansi 30 wanaochukua taarifa za mvua kila siku na taarifa za unyevu kwa kila wiki. Hii imeongeza nguvu ya ushirikishwaji na umiliki wa huduma za mradi, unaoruhusu urekebishaji na uthibitishaji wa muundo wa taarifa za hali ya hewa.



Mradi huu umefadhiliwa na



Wasiliana nasi

Meneja wa Mradi: lorenzo.occelli@weatherimpact.com
Mratibu wa Mradi Tanzania: bkadikilo@tyegd.org

@kilimothabiti